masomo ya biblia kwa njia ya posta ya wakristadelphiano. Na 9.

UFALME WAKO UJE

Somo: 1 Nyakati 29

> *"Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni"*

Ni mara ngapi umeyasema maneno haya, au umeyasikia na wengine? Maneno haya ni sehemu ya sala ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake. Unaweza kuyasoma katika Luka 11:2-4. Tunayajua maneno haya vizuri sana lakini je tunajua yanavyo maanisha?

Yaangalie tena. Ni maneno ya sala kwamba Ufalme wa Mungu uweze kuja, na kwamba mapenzi yaweza *kutimizwa hapa duniani,* kama yanavyotimizwa daima mbinguni. Kwa hiyo tunaona moja kwa moja kwamba ufalme tunaouomba utakuwa hapa katika dunia hii. Na hapa Ufalme wa Mungu utakapokuja, ndipo wanaume na wanawake watakapofanya mapenzi yake.

Nchi ya Ufalme huo

Ufalme ni lazima uwe *mahali fulani,* na kwa maelfu ya miaka iliyopita Mungo alichagua nchi ambayo ingekuwa Makao Makuu ya Ufalme wake. Hii ni nchi ya Israeli.
Yerusalemu ni Makao Makuu ya Israeli na baadaye utakuwa Makao Makuu ya ulimwengu wakati Yesu Kristo atakapokuwa anatawala kama Mfalme. Yesu mwenyewe alisema:

> *"Lakini mimi nawaambia, Usiape kabisa; hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu; wala kwa nchi, kwa maana ndiyo pakuwekea miguu yake; wala kwa Yerusalemu, kwa maana ndio mji wa Mfalme Mkuu" (Mathayo 5:34-35).*

Yesu aliyanukuu maneno haya kutoka Zaburi 48, ambayo ni kielelezo kwetu kwamba tuwe tunasoma pia Agano la Kale. Kifunu cha 2 cha Zaburi 48 kinasema:

> *"Kuinuka kwake ni mzuri sana. Ni furaha ya dunia yote. Mlima Sayuni pande za Kaskazini, Mji wa Mfalme Mkuu..."*

Mlima Sayuni ni sehemu ya Yerusalemu. Angalia ya kwamba umeelekezwa kama, *"Ni furaha ya dunia yote".*

Zaburi 2 inasema:

> *"Nami nimemweka mfalme wangu. Juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu" (mstari wa 6)*

Zaburi hii ni utabiri wa wakati Yesu atakapotawala kutoka Mlima Sayuni, kilimi cha Yerusalemu. Mungu alichagua kuliweka jina lake katika jiji la Yerusalemu. Tunayaona haya katika 2 Nyakati 6:5-6.

> *"Lakini nimeichagua Yerusalemu, jina langu liwe humo ... "*

Hapa kuna vifungu viwili zaidi kwa ajili yako kuvisoma kwa uangalifu:

(a) Isaya 62:1-7. Hapa tunaambiwa kumwomba Mungu aufanye Yerusalemu kuwa sifa duniani.
(b) Isaya 65: 17-25, ambapo Mungu anaandaa mpango wake na Yerusalemu na kutuambia
tufurahie.

11A (a) Maana yake nini 'kutokufa' katika Biblia?
(b) Ni nani watakaoishi milele?
(c) Watu wasio kufa watamsaidia Bwana Yesu Kristo kufanya nini?
(d) Muda wa Ufalme ujao, watu wataishi wapi - mbinguni au duniani?

11B *Kazi ya ziada* Unafikiria namna gani Ufalme wa Mungu duniani utafananaje? (Tumia Zaburi 72 na Isaya 35 ili kukusaidia.)

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

Karatasi Ya Maswali

Jaribu na ujibu maswali kwa maneno yako mwenyewe. Mahali inaposema "kazi ya ziada" unaweza kujibu swali au kuacha kama utaona ni magumu mno. Tafadhali jaribu kujibu maswali yote. Kumbuka kuweka jina lako, anuani na namba juu ya kila karatasi ya majibu.

MASOMO 9 –11

9A Ufalme wa Mungu wakati uliopita:
- (a) Ulikuwa wapi?
- (b) Ni nani aliyekuwa ni Mfalme wake wa kweli aliyetoa sheria?

9B Ufalme wa Mungu kwa wakati ujao:
- (a) Utakuwa wapi?
- (b) Ni nani atakuwa Mfalme?
- (c) Ni mji wake upi mkuu?
- (d) Itakuwa lini?

10A Andika jina la mtu aliye sahihi! (Majina yote yaweza kupatikana katika Somo la 10.)
- (a) Aliokolewa toka kufa maji kwa sababu alimtii Mungu.
- (b) Malaika wa Mungu alimtokea katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto.
- (c) Kuna nchi iliyoitwa baada yake.
- (d) Alikuwa ni mfalme wa kwanza wa Israeli.
- (e) Mfalme huyu aliota ndoto inayohusu madola ya ulimwengu wakati ujao.
- (f) Aliiacha nyumba yake, nchi na jamaa kwa sababu Mungu alimwambia hivyo.
- (g) Alisimama badala ya jiwe katika ndoto iliyohusu sanamu.
- (h) Mara baada ya utawala wake, Ufalme wa Israeli uligawanyika katika sehemu 2.
- (i) Alikuwa ni mtu wa kwanza kumuasi Mungu.

10B (a) Sehemu gani ya sanamu ambayo aliiona Nebukadreza katika ndoto inayotaja siku zetu?
- (b) Kwa sababu gani ni maelezo mazuri ya siku zetu?

Kulikuwepo na Ufalme wa Mungu duniani

Je ulijua kwamba, maelfu ya miaka iliyopita, Ufalme wa Mungu ulikuwepo kilhalisi duniani? Rudia tena katika 1 Nyakati, sura ya 29, na soma mstari wa 1, halafu mistari 10 - 13, ukiangalia kwa makini mstari wa 11, unaosema:

> *"Ufalme **ni wako**, Ee Bwana, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote"*

Ufalme unaozungumziwa, kama utakavyoona utakaposoma sura hijo, ni Ufalme wa Israeli, katika nchi ya Israeli. Sasa soma mstari wa 23,

> *"Ndipo Sulemani akaketi katika kiti cha enzi cha Bwana, awe mfalme badala ya Daudi babaye".*

Kiti cha enzi ambacho Daudi alikalia, na ambacho mwanaye Sulemani alikikalia baada yake, kilikuwa *Yerusalemu,* mji Mkuu katika nchi ya Israeli. Na Ufalme aliokuwa akiutawala ulikuwa Ufalme wa Israeli.

Kwa nini Ufalme wa Israeli uliitwa Ufalme wa Mungu, na kwa nini kiti chake kiliitwa "Kiti cha enzi cha BWANA" ? Ilikuwa kwa sababu

* Mungu mwenyewe aliwapa Waisraeli Ufalme huo
* Aliuchagua Yerusalemu kuwa mji Mkuu (1 Fal. 11:13)
* Alitoa sheria ambazo kwa hizo Ufalme ungetawaliwa (vitabu vya Walawi, Hesabu na kumbukumbu ya Torati)
* Mfalme alikuwa anatawala kwa niaba ya Mungu.

Ufalme wa Mungu wapinduliwa

Mamia ya miaka ilipita. Mfalme baada ya Mfalme walitawala juu ya Israeli kutoka Yerusalemu. Wengine walikuwa wafalme wazuri, wakitawala kwa kumwogopa Mungu, na wengine walikuwa waovu.

Mwishoni siku ilifika ambapo taifa la Israeli liliondoka kwa umbali mkubwa sana kutoka njia za Mungu, na mfalme aliyekuwa anatawala katika Yerusalemu alikuwa mwovu mno, kiasi kwamba Mungu alisema kwamba Ufalme huo usiendelee zaidi.

Soma Ezekieli 21: 25-27, na haswa mstari wa 27, unaosema:

“Nitaipindua, nitaipindua, nitaipindua; hiki nacho hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake; nami nitampa.”

Yeye ambaye ni haki yake

Tunaweza kuona kutoka vifungu katika Ezekieli kwamba mtu fulani angekuja ambaye “alikuwa na haki” kwa cha Ufalme wa Mungu - Yeye ambaye alikuwa mrithi - na Mungu angekuja kumpa kiti hicho.
Tokea siku ambapo mfalme wa mwisho aliondolewa kwenye kiti, mpaka siku ya leo, hajawahi kuwepo Wayahudi anayetawala katika Yerusalemu.

Lakini fungua yako katika Luka 1:31 - 33 na usome maneno yaliyosemwa na malaika kwa Mariamu mamaye Yesu. Akizungumzia Yesu, Malaika alisema:

“Huyo atakuwa Mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake”.

Ni na aliye na haki kwenye kiti cha Ufalme wa Mungu? Bila shaka ni Yesu, Mwana wa Mungu. Kwa kweli ana haki kwa njia mbili,

1. Kwa sababu ni Mwana wa Mungu;
2. Kwa sababu Mariamu mamaye alikuwa uzao wa Mfalme Daudi.

Kuna kutoeleweka kwingi kuhusu utawala wa Yesu katika Ufalme wa Mungu. Ni muhimu kutambua kwamba:

* Yesu atatawala katika dunia hii
* Kiti chake kitakuwa kiti cha Daudi katika Yerusalemu
* Yerusalemu utakuwa Makao Makuu ya Ufalme wa Mungu katika dunia.

Hii ndiyo sababu Yesu atarudi duniani. Kusudi la Mungu lipo pamoja na mwanadamu juu ya dunia na atatimiza kusudi hilo:

“Tena kama dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA” (Hesabu 14:21).

11A (a) Maana yake nini 'kutokufa' katika Biblia?
(b) Ni nani watakaoishi milele?
(c) Watu wasio kufa watamsaidia Bwana Yesu Kristo kufanya nini?
(d) Muda wa Ufalme ujao, watu wataishi wapi - mbinguni au duniani?

11B *Kazi ya ziada* Unafikiria namna gani Ufalme wa Mungu duniani utafananaje? (Tumia Zaburi 72 na Isaya 35 ili kukusaidia.)

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

Karatasi Ya Maswali

3

Jaribu na ujibu maswali kwa maneno yako mwenyewe. Mahali inaposema "kazi ya ziada" unaweza kujibu swali au kuacha kama utaona ni magumu mno. Tafadhali jaribu kujibu maswali yote. Kumbuka kuweka jina lako, anuani na namba juu ya kila karatasi ya majibu.

MASOMO 9 –11

9A Ufalme wa Mungu wakati uliopita:
- (a) Ulikuwa wapi?
- (c) Ni nani aliyekuwa ni Mfalme wake wa kweli aliyetoa sheria?

9B Ufalme wa Mungu kwa wakati ujao:
- (e) Utakuwa wapi?
- (f) Ni nani atakuwa Mfalme?
- (g) Ni mji wake upi mkuu?
- (h) Itakuwa lini?

10A Andika jina la mtu aliye sahihi! (Majina yote yaweza kupatikana katika Somo la 10.)
- (a) Aliokolewa toka kufa maji kwa sababu alimtii Mungu.
- (b) Malaika wa Mungu alimtokea katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto.
- (c) Kuna nchi iliyoitwa baada yake.
- (d) Alikuwa ni mfalme wa kwanza wa Israeli.
- (e) Mfalme huyu aliota ndoto inayohusu madola ya ulimwengu wakati ujao.
- (f) Aliiacha nyumba yake, nchi na jamaa kwa sababu Mungu alimwambia hivyo.
- (g) Alisimama badala ya jiwe katika ndoto iliyohusu sanamu.
- (h) Mara baada ya utawala wake, Ufalme wa Israeli uligawanyika katika sehemu 2.
- (i) Alikuwa ni mtu wa kwanza kumuasi Mungu.

10B (a) Sehemu gani ya sanamu ambayo aliiona Nebukadreza katika ndoto inayotaja siku zetu?

(b) Kwa sababu gani ni maelezo mazuri ya siku zetu?

Haitokani na Maandiko, wala hailingani na mafundisho ya Maandiko, kufikiri kwamba mwanadamu anaenda mbinguni wakati wa mauti, wala kwamba Ufalme wa Mungu upo mbinguni. Ni dhahiri kwamba Mungu anatawala Mbinguni, lakini kusudi lake ni kumtuma Yesu ili aitawale dunia na wanafunzi wake waaminifu wa enzi zote watamsaidia katika kazi hii kuu.

Yesu alidai kuwa ni Mfalme. Wakati wa mashtaka, Pilato alipomwuliza, “Wewe U mfalme basi?” Yesu alijibu:

> *“Wewe wasema kwa kuwa mimi ni Mfalme” (Yohana 18:37).*

Hiyo ndiyo namna ya Waisraeli ya kusema, *“Ndiyo, ni mimi.”*

Juu ya msalaba waliomsulubishia paliandikwa, “HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI” (Mathayo 27:37). Maadui wake walikuwa na maana ya kumdhihaki, lakini walichosema kilikuwa ukweli.

Injili ambayo Yesu aliihubiri ilikuwa habari njema ya Ufalme wa Mungu. Katika Luka 8:1, tunasoma kwamba,

> *“Alikuwa akizunguka zunguka katika miji na vijiji akihubiri na kuitangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu.”*

Sasa unajua kwa nini Yesu anarudi. Anarudi kuanzisha tena Ufalme wa Mungu katika dunia.

KITI CHA DAUDI KATIKA YERUSALEMU		
UFALME WA ISRAELI		***UFALME WA MUNGU***
WAFALME JUU YA KITI Daudi, Sulemani	KITI KIKO WAZI Hakuna wafalme	YESU JUU YA KITI akiwa amerudi kutoka mbinguni kuanzisha Ufalme wa Mungu duniani
VITABU VYA SAMWELI NA WAFALME	EZEKIELI 21:27	LUKA 1:32
1000 K.K.	600 K.K. LEO	MBELENI

Ufalme na sisi wenyewe

Labda unaweza kufikiri, “Kwa nini, tena, tuombe, ‘Ufalme wako uje’ ? Iwapo ni Ufalme wa Waisraeli, unatuhusu nini sis?”

Utajifunza, kadri unavyoendelea na masomo yako, kwamba Ufalme ambao Yesu atatawala utaenea mbali zaidi ya Ufalme wa kwanza wa Mungu - hasa, utaenea duniani kote, na kuleta amani kwa watu **wote.**

Na hivyo hivyo tunasali, “Ufalme wako uje”. Na tunaomba, pia, kwamba Yesu atakaporudi, anaweza kutuambia sisi:

> *“Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu” (Mathayo 25:34).*

Sura za kusoma: Mwanzo; Wagalatia 3

Muhtasari - angalia jinsi kila sehemu ya Biblia inavyosaidia kuelezea juu ya sehemu nyingine.

Sasa tumejifunza:

1. Kwamba Ufalme wa Mungu Uliwahi kuwepo katika nchi ya Israeli.
2. Kwamba Mungu aliukomesha ufalme huo, lakini aliahidi kuurejesha kwa mrithi mwenye haki.
3. Kwamba mrithi huyu ni Yesu, na atakaa kwenye kiti cha Daudi katika Yerusalemu, akiwatawala kwa pamoja Wayahudi na ulimwengu wote.
4. Kwamba waaminifu wote watashiriki katika baraka za Ufalme huo katika dunia

Jifunze kwa moyo: Ufunuo 11:15

> *“Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele.”*

"Miisho yote ya dunia itakukumbuka na kumrejea BWANA: na jamaa zote za mataifa watamsujudia. Maana Ufalme ni wa Bwana, naye ndiye anaye tawala kati ya mataifa.”



Ramani ya vipindi vya watu na Mungu

Ukamilifu mkubwa zaidi usio badilika
Umri wa Ufalme utadumu kwa miaka elfu. Itakuwa ni kipindi cha ajabu, lakini hiki kipindi hakitakuwa kamilifu. Wanaume na wanawake wa kawaida watakaoishi katika Ufalme watakuwa bado wanaumbile la asili la mwanadamu, ambalo ni rahisi kutenda dhambi. Bado watazeeka na kufa. Hata tunaambiwa kwamba mataifa mengine yatauasi utawala wa Bwana Yesu kwenye mwisho wa miaka elfu.

Bila shaka atawashinda kabisa. Wakati huo wale waliokuwa waaminifu katika kipindi cha Ufalme watapewa thawabu ya uzima wa milele. Wale ambao watakuwa wamekuwa wamekufa watafufuliwa kwa ajili ya hukumu na Yesu.

Kisha, dunia yote itajawa na utukufu wa Mungu, na Yeye - Muumba mkuu – atakuwa "yote katika wote' (1 Wakorintho 15:28).

Muhutasari
1. Yesu atakaporudi. atakuwa Mfalme wa ulimwengu.
2. Mji wake mkuu utakuwa ni Yerusalemu.
3. Ulimwenguni pote kutakuwa na amani na ustawi. afya na furaha.
4. Katika Ufalme wake utakao enea pote. kila mtu atajifunza kutii maagizo ya Mungu
5. Katika Ufalme kutakuwa na -
   (a) watu wasio kufa. waliomfuata Yesu nao wameisha tii amri za Mungu katika maisha yao. Wakiwa hawafi hawataugua tena au kufanya vita JUU ya dhambi. Watamsaidia Yesu na kuutunza ulimwengu na watu wake katika Ufalme wa Mungu.
   (b) watu wanaokufa waliopona hatari na hukumu ya Mungu ya kutisha juu ya ulimwengu mwovu. Watajifunza kumtii kwa kumtumikia na kumwabudu Mungu.

Sura za kusoma: Zaburi 72; Mika 4:1 – 7
Jifunze kwa moyo: Zaburi 22:27,28:

MTAZAMO WA MUNGU JUU YA HISTORIA

Na10.

Somo: Danieli 2

Mungu haiangalii historia kama sisi tunavyoiangalia. Utawala ambao watu wanaufikiria kwamba ni maarufu unaweza kuwa si lolote mbele ya macho ya Mungu. Kwa upande mwingine, mtu mkimya na mnyenyekevu anayepuuzwa na wenzake anaweza kuwa muhimu sana machoni pa Mungu.
Biblia ni kitabu cha Mungu cha Historia, na Wayahudi ni watu wake. Mpango wa Mungu wa wokovu ulikusudiwa kwa Wayahudi, ingawa unaenea kwa mataifa yote. Haishangazi, kwa hiyo, historia iliyomo ndani ya Biblia inajihusisha zaidi na Wayahudi.

Hapa kuna maelezo mafupi juu ya baadhi ya wanaume katika hadithi za Biblia.

ADAMU alikuwa mtu wa kwanza. Mungu alimfanya mzuri sana; lakini hakumtii Mungu. Tokea wakati huo mpaka sasa, wote hawamtii Mungu kwa njia moja au nyingine (Mwanzo 1 na 3). Na watu wote wamekufa.
NUHU alizaliwa zaidi ya miaka elfu moja baada ya Adamu. Wakati wa siku zake, watu waliongezeka uovu kiasi kwamba Mungu alituma gharika na kuwaangamiza wote, isipokuwa Nuhu na ukoo wake. Nuhu alimwamini Mungu na kumtii (Mwanzo 6).

IBRAHIMU anaitwa 'Rafiki wa Mungu' katika Biblia. Mungu alimwambia andoke katika nyumba yake katika Uru, na aende kuishi Kanaani, naye Ibrahimu alimtii Mungu. Mungu akamwahidi ahadi maalumu (Mwanzo 12).

ISAKA alikuwa mwana wa Ibrahimu, aliyezaliwa kwa mwujiza wakati Ibrahimu na mke wake walikwisha pita umri wa kuzaa watoto (Mwanzo 21).

YAKOBO alikuwa mwana wa Isaka. Mungu alimbadilisha jina lake kuwa Israeli, linalo maanisha 'mwana wa mfalme aliye pamoja na Mungu'. Yakobo alikuwa na wana kumi na mbili.

YUSUFU alikuwa mmoja kati ya wana kumi na wawili wa Yakobo. Kaka zake walimwongea wivu, na wakamwuza Misri kama mtumwa. Alipata majaribu mengi, lakini Mungu alimbariki, na akawa mtawala wa pili katika Misri.

Baadaye, uzao wote wa Yakobo ulimfuata Yusufu huko Misri (Mwanzo 46). Miaka mingi baadaye, walipofikia kuwa taifa la watu, walifanywa watumwa wa Wamisri.

MUSA alizaliwa na wazazi wa Kiyahudi, lakini alilelewa na binti wa Farao. Mungu alimtumia kuwatoa Waisraeli katika Misri, na kuwapeleka katika nchi ya Kanaani, ambayo aliwaahidi.

Mungu aliwapa watu hao sheria zenye hekima, lakini hawakuzitii, na hata waligeuka kuabudu sanamu.

SANAMU

Sanamu ni kitu cho chote kinacho abudiwa badala ya Mungu wa kweli. Watu wameabudu vitu vingi - jua, miti, vinyago, mawe, Sanamu za kuchongwa na vingine vingi. Hii ni miungu ya ***uongo*** na haiwezi kusaidia, kufikiri wala kutenda.

Baada ya miaka 400 hivi ya kutangatanga nyikani ambako watu wengi waliokuwa wakubwa walikufa kwa kukosa imani, hatimaye walifika katika nchi ambayo Mungu aliwaahidi.

YOSHUA aliwaongoza watu kuingia katika nchi iliyoahidiwa, nchi ya Kanaani.

Waamuzi wanatawala watu

Kwa muda wa miaka kama 400, Wayahudi walitawaliwa na Waamuzi katika nchi yao, lakini Mungu ndiye aliyekuwa Mfalme wao. Mara kwa mara hawakuzitii sheria Zake, na aliwaadhibu kwa kuyatuma mataifa yaliyowazunguka kufanya vita nao. Walipokuwa katika matatizo, watu walimgeukia Mungu, naye akawaokoa kupitia kwa mmoja wa Waamuzi.

Watu Wanahitaji Mfalme

Badala ya kuishi kwa furaha katika utiifu kwa Mungu, Wayahudi waliomba wawe na Mfalme. Hawakumtaka Mungu. Walitaka Mfalme ambaye wangeweza kumwona kama mataifa mengine.

Uponyaji wa akili na mwili

Pamoja na mibaraka hii itakuja pia baraka kubwa ya afya na nguvu.

Yesu alipoishi duniani karibu miaka 2000 iliyopita, alileta afya kwa wengi waliokuwa wagonjwa, kwa kutumia uweza aliopewa na Mungu. Katika Ufalme wa Mungu, uweza huu utaonekana tena. Soma Isaya 35:5:

> ***"Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Wakati huo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye Bubu utaimba."***

Tunaweza kuwazia vema, zaidi, yakuwa watu wanaokufa wataishi muda mrefu kuliko leo. Nabii Zekaria anatuambia kwamba jambo hili litakuwa hivyo. Anasema:

> ***"Wazee wanaume na wazee wanawake watakaa tena katika mitaa ya Yerusalemu, kila mtu ana mkongojo wake mkononi, kwa kuwa ni wazee sana. Na mitaa ya mji itajaa wavulana na wasichana wakicheza katika njia zake" (Zekaria 8:4,5).***

Mistari hii inazungumzia Yerusalemu, lakini, kama tulivyo ona, mibaraka ya Ufalme itaenea dunia yote.

La kweli neno la Mungu

Pengine unawaza, "Yote haya yanaonekana mazuri sana, lakini hapana budi kuwa mazuri mno na ni ya kweli". Ikiwa ahadi tulizo soma zinategemea watu, basi ni hapana shaka hatuwezi kuweka tumaini kwa hizo. Hata watu walio bora hawawezi kuwa na uwezo wa kutimiza wanayoahidi, kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu.

Bali ahadi hizi zatoka kwa Mungu, nasi twaweza kuziwekea tumaini. Soma Isaya 55:6-11, na utazame hasa mstari wa 11:

> ***"Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu, halitanirudia bure bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niniyolituma."***

Hivyo tuweze kutazamia na furaha kwa kipindi kile hapo utakapo kuwa "Utukufu kwa Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani" (Luka 2:14).

2 Wakati huo watakuwepo Wayahudi ambao wamemkubali Yesu kuwa Mfalme wao. Wataishi Israeli ambayo itakuwa ni nchi kuu ya ulimwengu:

> "Wakati ule watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha BWANA; na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu, kwa ajili ya jina la BWANA; wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao mbaya" (Yeremia 3:17).

Kristo atakuwa kati yao, nao watabarikiwa mno, ingawa watakuwa bado wanakufa (yaani wataweza kuendelea kufa).

3. Yesu atakapo kuja, hukumu ya Mungu itakuwa kali kwa maana watu wengi wataangamia. Bali wale watakao baki hai, ulimwenguni pote, chini ya utawala wa Yesu, watajifunza kufanya yale yanayompendeza Mungu - kama tunavyo ambiwa kwa Isaya 26:9:

"Wakati hukumu zako zikiwamo duniani, watu wakaao duniani watajifunza haki."

Ustawi kwa wote

Pamoja na hali ya mambo kuwa kamili ndipo wakati huo yatakuwepo mafanikio katika kila mkono. Zaburi 72:16 unasema:

"Itakuwepo nafaka ya kutosha katika nchi na katika ardhi juu ya milima; matunda yake yatawaya-waya kama Lebanoni."

Mara kwa mara vilele vya milima vipo tupu. Kama ikiwapo nafaka juu ya milima, tunaweza kuwaza ni kiasi gani cha nafaka itakayokuwa nyingi bondeni. Kama tunavyosoma tena katika Zaburi 67:6:

"Wakati huo nchi itatoa mazao yake; na MUNGU, Mungu wetu ametubariki."

Hata majangwa yatakuwa ya kijani katika siku hizo. Soma tena mistari ya kuvutia kwa Isaya 35:1, 2 inayotuambia jinsi -

"Jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi. Litachanua maua mengi, na kufurahi, naam, kwa shangwe na kuimba."

SAUL alikuwa Mfalme wa Kwanza. Hakumpendeza Mungu, naye hakuwa mtiifu. Mfalme wa pili.



DAUDI katika Biblia anaitwa, “mtu aupendezaye moyo wa Mungu.” Aliahidiwa ahadi maalum, ambazo zingetimizwa na Bwana Yesu (2 Samweli 7),

Daudi alifuatiwa katika kiti na mwanye, **SULEMANI,** lakini Israeli bado ilibaki kuwa Ufalme wa Mungu, kama utakavyoseoma katika 1 Nyakati 29:23:

“Ndipo Sulemani akaketi katika kiti cha enzi cha Bwana... “

Ufalme uliogawanyika

Baada ya Sulemani, Ufalme uligawanyika. Sehemu ya kaskazini uliitwa Israeli, na sehemu ya kusini uliitwa Yuda.

Watu wa Israeli, wa Kaskazini, waliendelea kuwa waovu kiasi kwamba Mungu aliwaleta Waasiria kushindana nao. Wakawakamata mateka, na hawakurudi kamwe kwenye nchi yao.

Ufalme wa Kusini, Yuda, haukutofautiana sana. Walichukuliwa mateka kwenda Babeli. Tokea wakati huo, hawakuwa na mfalme. Walirudi katika nchi yao, Israeli, baada ya miaka 70.

Agano Jipya

Hatimaye, kama miaka 400 baada ya kufunga kwa Agano la kale, Mungu alimtuma mwanaye, Bwana Yesu Kristo. Agano Jipya linasimulia habari za Yesu, na mwanzo wa kanisa la Kikristo.

Wengi wa wananchi wenzake, yaani Wayahudi, walimkataa Yesu. Hatimaye Mungu akatoa ahadi ya uzima kupitia kwa Yesu kwa watu wa mataifa yote; tunasoma jinsi Wakristo wa kwanza walivyosafiri kwenda mbali wakihubiri njia hii mpya ya uzima. Mahubiri hayo yanaendelea hata leo.

Maono ya Falme za Ulimwengu

Kabla hujajifunza sehemu hii, ichunguze kwa ungalifu picha ya hapa chini. Maono haya yameenea historia ya ulimwengu kuanzia wakati wa Babeli, mpaka wakati wa siku zetu na hata mbeleni. Inaonyesha jinsi Mungu, kwa pomoja, anavyojua na kuongoza serikali, nchi na mataifa na anavyotoa ishara ya Ufalme wa Mungu utakapokuja.

Je unakumbuka jinsi Waisraeli walivyochukuliwa mateka kwenda Babeli? Miongoni mwa waliochukuliwa alikuwemo kijana wa uzao wa Kifalme aliyeitwa **DANIELI.**

Usiku mmoja **NEBUKADNEZA** mfalme wa Babeli, aliota ndoto ya ajabu. Ndoto hii ilitumwa na Mungu, na Mungu alimwonyesha Danieli tafsiri yake.

Mfalme aliona sanamu kubwa sana, kitu kama picha hii. Sanamu hiyo ilisimama badala ya falme kubwa nne, falme za Babeli, Umedi-Uajemi, Uyunani, na Rumi, ambazo zote zingeshamiri kwa wakati, halafu moja baada ya nyingine, zingetoweka. Haya yote yalitendeka na tunaweza kusoma habari hizi katika vitabu vya historia.

Kichwa cha dhahabu cha sanamu hiyo kiliwakilisha ufalme wa Babeli, ambao ulikuwa tajiri sana. Kifua cha Sanamu kilitengenezwa kwa fedha na kiliwakilisha ufalme wa Umedi na Uajemi. Halafu likaja tumbo na viuno vya shaba, ambavyo viliwakilisha ufalme wa Uyunani.

Mwishoni ufalme wa Kirumi ulikuja kuutawala Ulimwengu. Ufalme huo uliwakilishwa na miguu ya chuma-chuma kwa sababu ulikuwa ufalme mgumu na wa kikatili, na pia ulikuwa na nguvu sana. Ufalme wa Kirumi ulipanuka zaidi kuliko falme nyingine na ulitoa sheria kwa ulimwengu ambazo ni msingi wa sheria nyingi leo. Ilikuwa ni wakati wa Ufalme wa Rumi ambapo Bwana Yesu alizaliwa, na walikuwa ni maaskari wa Kirumi waliomsulubisha. Mamia ya miaka baadaye Ufalme wa Kirumi ulivunjika na tangu hapo hapajatokea ufalme wa duniani unaotawala ulimwengu tunaoufahamu.

Ufalme usio na upungufu

Hebu fikiri ulikuwa umeulizwa useme ni hali gani ungependa kuishi katika ulimwengu usio na kombo lolote.

Moja ya mambo ya kwanza ambayo ungeomba itakuwa ni usalama; uhuru wa kutoka kwenye hofu, na amani ili kufurahia matunda za kazi yako. Kwa kweli, huenda utakuwa na picha katika fikra zako, jambo lingine kama hili moja atupalo sisi nabii Mika:

> ***"Naye (huyo ni Yesu Kristo) atafanya hukumu kati ya watu wengi, atawakemea mataifa wenye nguvu walio mbali; nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu: taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe. Bali wataketi kila mtu chini ya mzabibu wake na chini ya mtini wake, wala hapana mtu atakayewatia hofu: kwa kuwa kinywa cha BWANA wa majeshi kimesema hivi." (Mika 4:3,4)***

Lakini kabla ya kuweza kuwapo amani, inabidi iwepo bidii ya kweli kwa upande wa watu kuenenda katika njia za Mungu. Kwa muda wanapoendelea kwenda njia yao itakuwapo shida. Hivyo moja ya kazi za Bwana Yesu itakuwa kuwafunza mataifa yote njia za Mungu.

Lakini unaweza kusema, yatakuwapo mataifa mengine ambayo hayatasikiliza ! Hiyo ni kweli, na wale ambao hawatatii wataadhibiwa, kama tunavyosoma kwa Isaya 11:4:
"Kwa pumzi ya midomo yake atawaua wabaya"

- maana, ukumbuke, hapo Yesu ajapo atakuwa ni mwenye nguvu zote.

Ni nani watakuwamo katika Ufalme?

1. Kwanza, watakuwapo viongozi. Watakuwepo wanaume na wanawake waliokuwa ni wanafunzi, wafuasi wa Yesu, wa kutoka nyakati zote, ambao sasa wanakuwa wamepewa uzima wa milele Yesu akija. Watakuwa ni wafalme na makuhani, wakimsaida Yesu kutawala ulimwengu. Watakuwa ni watu wasio kufa tena.

   "Nao waimba wimba wimbo mpya, wakisema, Wastahili wewe kukitwa hicho kitabu na kuzivunja muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, umemnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila, jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani, nasi tutamiliki juu ya nchi" (Ufunuo 5:9,10).

Na 11.

Kusoma: Isaya 35

Yesu alipozaliwa, malaika walaika waliimba kwa furaha. Maneno ya wimbo wao umeandikwa kwa Luka 2:14:

"Utukufu kwa Mungu juu, na duniani amani kwa watu aliowaridhia."

Bado tangu siku ile mpaka leo, kamwe haijakuwepo amani ya kweli ya kudumu kwa dunia, na haitakuwapo kamwe, mpaka Yesu arudi duniani kuweka Ufalme wa Mungu.

Agano la Kale linatuambia mengi kuhusu Ufalme, nalo linatupa picha nyingi za kipindi cha amani na ustawi utawi utakao kuja.

Eneo la Ufalme

Angalia tena Zaburi 72. Katika Zaburi hii tumepewa picha kwa maneno ya kipindi hapo Ufalme wa Mungu utakapokuwa umesimamishwa duniani. Lakini, kwa kitambo kidogo, tazama hasa mstari wa 8:

"Atatawala pia kutoka bahari hata bahari, na kutoka mto mpaka miisho ya duniani."

Hapa tunaambiwa kwamba Ufalme utakaosimamishwa na Yesu, kitovu chake kikiwa Israeli, utaenea juu ya dunia yote. Twalipata jambo lilo hilo katika Zaburi 2:8, mahali anapomtaja Yesu, kusema:

"Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa miliki yako ..."

Tutazame zaidi mstari. Zekaria sura ya 14, soma mstari wa 9:

*"Naye Bwana atakuwa Mfalme **juu ya dunia yote:** katika siku ile Bwana takuwa mmoja, jina lake moja."*

Utawala wa Kristo

Yesu Kristo atatawala kutokea Yerusalemu, mji wake mkuu, ambao aliwahi kuuita *"mji wa Mfalme Mkuu"* (Mathayo 5:35). Sheria zake zitakwenda kwa mataifa yote, kame tunavyosoma kwa Isaya 2. Soma mistari 1-4, na angalia hasa:

"Katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana kutoka Yerusalemu."



Kichwa cha dhahabu
BABELI
Kama 600 K.K.

Kifua na mikono ya fedha
UMEDI UAJEMI
Kama 450 K.K.

Tumbo na Viuno vya Shaba
UYUNANI
Kama 300 K.K.

Miguu ya Chuma
RUMI
Mwanzo wa Ukristo

Nyayo za Miguu za Chuma na Udongo

Kwa muda wa miaka 1500 imekuwa ni wakati wa nyayo za miguu katika ile sanamu, mchanganyiko wa chuma na udongo, mataifa yenye nguvu na mataifa yasiyo na nguvu. Hivyo ndivyo ilivyo leo.

Ndipo, katika ndoto, Nebukadneza akaona jiwe dogo, *"Likachongwa bila kazi ya mkono".* Jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, na likaivunja vipande. Ndipo, lile jiwe likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia.

Jiwe hilo, *"lililochongwa bila kazi ya mkono"* linasimama badala ya Yesu, ambaye hakuwa na baba wa kibinadamu. Atakaporudi, ataangamiza kabisa falme za wanadamu, na kuusimika Ufalme wa Mungu, ambao utatapakaa duniani kote.

Hivi sasa tunaishi katika wakati wa chuma na udongo - wakati wa mgawanyiko. Mataifa mengine yana nguvu na mengine mengi ni dhaifu, na yanaelewana kidogo sana. Yamegawanyika na kuachana - kwa jinsi ambavyo vipande vya chuma havitangamani au kuchangamana na udongo. Upesi Yesu atarudi. Ataziangamiza falme za wanadamu, na kuuanzisha Ufalme wa Mungu, utakaoenea dunia yote.

Kiasi kikubwa cha yale yaliyoelezwa katika ndoto ya Nebukadneza yamekwisha tokea; tunaweza kuwa na uhakika kwamba sehemu ya mwisho vile vile itatekelezwa. Kumbuka kwamba Ufalme utakaokuja utakuwa hapa duniani.

Muhtasari

1. Agano la kale linatusimulia historia ya watu wa Mungu walioteuliwa - Wayahudi.
2. Agano Jipya linamhusu Yesu, na linatusimulia jinsi Injili ilivyohubiriwa kwa mataifa yote baada ya ufufuo wa Yesu.
3. Katika Agano la Kale kwa Agano Jipya kama tulizosoma kumbuka Kristo atakaporudi duniani kuanzisha Ufalme wa Mungu.
4. Utabiri wa Danieli 2 unaonyesha jinsi ambavyo falme kubwa nne zingefuatana katika historia. Tunaishi katika wakati wa "vidole" na tunamngojea Yesu (aliyeonyeshwa kama jiwe) kurudi tena.

Sura za kusoma : Kuna sura nyingi zilizotajwa katika somo hili. Jaribu kuzisoma zote: zitasaidia ufahamu wako. Ndipo usome Matendo 7.

Mstari wa kujifunza: Danieli 2:44

"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa Mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele."

Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN5 6DG

ISBN 1 902059 05 -0
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 9-11
Correspondence Course Lessons 9-11